**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

Namba za simu
Mkuu wa Shule **0765397438**

Shule ya Sekondari Unyahati
S.L.P 339,
**IKUNGI - SINGIDA**

Tarehe …………………..

Makamu Mkuu wa Shule **0628129501**

Mzazi/ Mlezi wa Mwanafunzi………………………………………………………………
S.L.P………………………………
…………………………………………………….

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI UNYAHATI ILIYOPO HALMASHAURI YA WILAYA YA IKUNGI MKOA WA SINGIDA KWA MWAKA WA MASOMO MWAKA 2024/2025**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika Shule ya Sekondari Unyahati **2024/2025** kwa tahasusi ya **CBG**

Shule ya Sekondari **Unyahati** ipo Ikungi karibu kabisa na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Ikungi na Mkabala Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ikungi. Shule ipo kilometa mbili (2 km) mashariki mwa mji wa Ikungi uliyopo katika Barabara Kuu ya Dodoma – Mwanza kupitia Singida. Kwa wanafunzi wanaotokea Kanda ya Ziwa (Mwanza, Mara, Bukoba, Shinyanga, Geita na Simiyu) hakikisha unashukia Standi ya Ikungi **baada** ya kupita Singida Mjini kuelekea Dodoma. Wanafunzi wanaotokea Mikoa ya Dodoma, Morogoro, Dar Salaam, Iringa na mikoa ya kusini manelekezwa kushukia Standi ya Ikungi **kabla** ya kufika Singida Mjini. Usafiri kutoka stendi hadi shuleni ni wa **pikipiki** Nauli ni shilingi **1,500/=**. Usafiri wa Pikipiki unapatikana katika kituo cha Mabasi cha Ikungi.

Muhula wa masomo unaanza tarehe **..................** Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **...................** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **........................................**

## 2.MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1 Sare za shule

Shule hii ni ya **Bweni** na ni ya **Wavulana pekee** hivyo sare ya shule ni kama ifuatavyo:

(i) Shati mbili nyeupe za tetroni mikono mirefu.
(ii) Suruali mbili za rangi ya **"Nyeusi" (blank)**. Suruali hizi zishonwe bila kuwekewa Marinda, pia isiwe ya kubana wala mdomo wa chupa miguuni.
(iii) Viatu vyeusi vya kufunga na kamba na vyenye visigino vifupi.
(iv) Soksi jozi mbili nyeusi
(v) Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali.
(vi) Nguo za kushindia (shamba dress) ni suruali mbili za kitambaa cha **Khaki**.
(vii) Mwanafunzi aje na Sweta (Bluu Bahari), T-shirt na Tai 2 nyeusi yenye mistari myeupe.
(viii) Mwanafunzi aje na jezi moja ya michezo yaani bukta na "T-shirt" damu ya Mzee (zinapatikana shuleni kwa Tshs 12,000/=)

Mwanafunzi haruhusiwi kufika shuleni na nguo nyingine yeyote tofauti na hizo alizoagizwa kwenye barua ya maelekezo. **Mwanafunzi afike shuleni akiwa amevaa suruali ya khaki na shati nyeupe ya mikono mirefu.**

### 2.2 Michango ya shule

(a) Fedha za michango zilipwe kwenye Akaunti ya shule **Na 50801100148** katika Benki ya **NMB** jina la akaunti ni **Unyahati Secondary School** (tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye "bank pay in slip" na ainisha malipo mfano tahadhari Tsh **5,000/=,** Nembo Tsh **5,000/=** n.k kisha kabidhi bank pay in slip halisi kwa mhasibu na ubaki na nakala yako

(b) **Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi kwa kila Mwanafunzi ni :-**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000.00 |
| 3. | Tahadhari | 5,000.00 |
| 4. | Nembo | 5,000.00 |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000.00 |
| | **Jumla ya michango yote** | **80,000.00** |

**Michango hii ilipiwe kupitia benki ya NMB kwenye akaunti namba 50801100148**

### 2.3. Mambo mengine ya kuzingatia

**(a) Mambo mengine ya kuzingatia kwa mwanafunzi ni kama ifuatavyo:-**

(i) Hakikisha mwanao ana kadi hai ya Bima ya Afya **NHIF** na kama hiyo bima itashindikana aje na passport saizi moja na Tsh 10,000/= kwa ajili ya kupatiwa CHIF kutoka Hospitali ya Wilaya ya Ikungi iliyopo karibu kabisa na shule.
(ii) Hakikisha mwanao anaripoti na godoro lenye inchi mbili na nusu na mapana na urefu tatu kwa sita(2 ½ na 3x6)
(iii) Mwanao anapoharibu mali ya shule atatakiwa kulipa gharama za utengenezaji.
(iv) Tunapendekeza mzazi kutupatia namba ya simu yenye whattsap kwa ajili ya taarifa muhimu za maendeleo ya mwanao na ya shule

**(c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-**

(i) Ream mbili (2) za A4 kwa mwaka zitakazopokelewa shuleni na Ream moja ambayo atabaki nayo mwanafunzi kwa ajili ya mazoezi atakayopewa na walimu**.**
(ii) Scientific calculator
(iii) Disection kit kwa wanafunzi wa somo la Biolojia
(iv) Mashuka mawili "Light blue", Blanket 1 na chandarua
(v) Vyombo vya chakula (Bakuli lenye mfuniko **(container)**, kijiko na kikombe)
(vi) Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko moja iitakabidhiwa shuleni na nyingine atabaki nayo mwanafunzi kwa matumizi yake binafsi
(vii) Chelewa moja kwa mwanafunzi kwa kila mwaka
(viii) Jembe na mpini wake, Rubber squeezer mbili (2), Hard broom moja (1) na soft broom moja (1)

**2.4 Sheria na Kanuni za Shule**

(i) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
(ii) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
(iii) Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
(iv) Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
(v) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
(vi) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
(vii) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
(viii) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
(ix) Kutunza mali za shule;
(x) Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
(xi) Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**3.1 MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**

(i) Wizi
(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku **90** bila taarifa/ utoro.
(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo.
(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla.
(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
(vi) Kunyoa nywele kwa mtindo usiokubalika na kufuga ndevu. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wawapo shuleni,huduma ya kunyoa inapatikana shuleni.
(vii) Ulevi au unywaji pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
(viii) Uvutaji wa sigara.
(ix) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
(x) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
(xi) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
(xii) Kumiliki kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
(xiii) Kudharau Bendera ya Taifa.
(xiv) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
(xv) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.
(xvi) Kushiriki matendo ya uhalifu, uchochezi wa kisiasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
(xvii) Kutoka nje ya Shule bila ruhusa ya Mwalimu.

**MUHIMU:**

**(a) Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

**(b) Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

**4 VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU**

(a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga wa hospitali ya Serikali)

(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.

(c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni kulipa michango na kutekeleza maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

(d) Picha (Passport size) nne (4). Mbili za Wazazi/Walezi yaani moja moja na mbili za Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

(e) Nakala mbili za cheti cha kuzaliwa

(f) Hati ya matokeo ya kidato cha nne (Result slip) halisi 1 na nakala 2

5 Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu. Mwanafunzi atasajiliwa tu baada ya kutekeleza maagizo haya na kukabidhi fomu zilizojazwa kikamilifu na si vinginevyo.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

*VGMmbaga*

**VICTOR GENESIS MMBAGA**
**MKUU WA SHULE**
**0765397438**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

Mkuu wa shule**: 0765397438**
Makamu Mkuu wa Shule: **0628129501**
Mwandamizi Taaluma**: 0717013274**
Mlezi wa Wanafunzi wa Kiume: **(Patron) 0768655704**

**KIAMBATANISHO A.**

**FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI UNYAHATI**
**A: SEHEMU YA MWANAFUNZI**
**MWANAFUNZI AJAZE SEHEMU HII**

1. Mimi ---------------------------------------------------------- ninakubali kujiunga na Shule ya Unyahati Sekondari katika Kidato cha ------------- kwa machaguo ya(combination) ---------

2. Mimi Mwanafunzi wa Unyahati Sekondari, ninakubali kwamba:
   (i) Nitafika Shuleni siku ya kufungua na bila kuchelewa kila muhula
   (ii)Nitatii sheria zote za shule pamoja na kutoshiriki katika ulevi, migomo na migogoro ya aina yeyote.
   (iii)Sitaleta shuleni wala kuvaa mavazi yasiyo ya heshima k.m. nguo za kubana, kofia, miwani ya giza, pete za urembo.
   (iv)Nitatumia juhudi na maarifa yote kujiimarisha kitaaluma ikiwa ni pamoja na kuhudhuria vipindi na kufanya mazoezi na mitihani yote (k.v. usafi na elimu ya kujitegemea).

   Saini ya Mwanafunzi --------------------------------- Tarehe -------------------------------

**B: SEHEMU YA MZAZI / MLEZI**
**MZAZI / MLEZI AJAZE SEHEMU HII**

1. Mimi ------------------------------------------------------------------nimekubali mtoto wangu ----------------

   ---------------------------------------------------ajiunge na Shule ya Sekondari Unyahati kuanzia

   tarehe ----------------------------.

   Ninaahidi kwamba:

(i) Nitawasaidia walimu kumlea mwanangu kitaaluma na kitabia. Nitamuonya na kumsisitiza mwanangu kutii sheria zote za shule na kuishi maisha mazuri kwa maadili ya kiuanafunzi.

(ii) Nitamkataza kuvaa nguo zisizo za heshima k.m. nguo za kubana, kofia, miwani ya giza n.k.

(iii) Nitampatia mtoto wangu nauli ya kuja shuleni na kurudi likizo bila kuchelewa.

(iv) Nitahakikisha anakuja shuleni siku ya kufungua kila muhula bila kuchelewa.

2. Anwani yangu ya kudumu

   --------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

   --------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

   ------------------------------------------------------------------------------------------

   Sahihi ya Mzazi / Mlezi -------------------------------------------- Tarehe-------------------------

**(Tafadhali njoo na fomu hii unapokuja shuleni ikiwa imejazwa).**

**KIAMBATANISHO B.**

**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**

**SHULE YA SEKONDARI UNYAHATI**

**FOMU YA MAELEZO BAYANA (PERSONAL PARTICULARS)**

**KWA AJILI YA USAJILI IJAZWE NA MZAZI / MLEZI**

1. Jina kamili la mwanafunzi kama alivyojiandikisha kwenye mtihani wa Kidato cha Nne--------------------------------------------------------------------------------
2. Jina kamili la Baba / Mlezi --------------------------------------------------------------------

(a) Anwani ya Baba / Mlezi ------------------------------------------------------------------

(ii) Namba ya simu ya Baba / Mlezi kazini---------------------------------------------

Nyumbani -------------------------------------------------------------------------------------

(iii) Mtaa / Kijiji ------------------------- Kata ------------------------Tarafa-------------------

Wilaya ------------------------------------------- anakokaa.

3. Jina la Mama / Mlezi -------------------------------------------------------------------------

(i) Anwani ya Mama / Mlezi ----------------------------------------------------------------

(ii) Namba ya simu ya Mama / Mlezi ----------------------------------------------------

Nyumbani -------------------------------------------------------------------------------------

(iii) Mtaa / Kijiji --------------------- Kata-------------------------- Tarafa-------------------

Wilaya ------------------------------------------------------- anakokaa.

4. Tarehe ya kuzaliwa mwanafunzi---------------------------------------------------------
5. Mahali alipozaliwa -------------------------------------Mkoa ---------------------Wilaya--------------------------------Kijiji / Mtaa-------------------------------------------
6. Kazi ya Baba / Mlezi --------------------------------------------------------------------------
7. Kazi ya Mama / Mlezi -----------------------------------------------------------------------
8. Je mwanafunzi anacho kilema chochote? ------------------------------------------

   Kijaze---------------------------------------------------------------------------------------------
9. Taja ndugu watatu ambao wanaweza kutoa msaada kwa mwanao

| NO. | JINA KAMILI | KAZI | UHUSIANO | NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |

**TAREHE --------------------------------SAHIHI YA MZAZI / MLEZI ----------------**

8.

**APENDIX 'A'**

**KIAMBATANISHO C**

**GOVERNMENT OF TANZANIA**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**PART A:**

TO: The Medical Officer From:-------------------------------------------------------
-------------------------------------------- ---------------------------------------------------
-------------------------------------------- ---------------------------------------------------
-------------------------------------------- ------------------------------------------------------

Mr. / Mrs. /Miss------------------------------------------------------------------------------------------------------------

**(Name in full)**

Please examine the above named as to his / her physical and mental fitness for a full – time Advanced Level of Secondary Education studies. The examination should include the following ineligible in case of a defect.

I. (a) Eyesight
   (b)Hearing
   (c)Speech
   (d)Limbs
   (e)Vuneral Diseases
   (f)Leprosy
   (g)Epilepsy
II. Neuroses
III. Other serious diseases

Date: ------------------------------------------------ Signature: ----------------------------------

**PART B:** **MEDICAL CERTIFICATE**
**(To be completed by a Government Officer)**

I have examined the above - named and consider that he /she is physically fit / unfit and mentally fit / unfit for a full – time Advanced Level of Secondary Education studies.

I. a) Eyesight--------------------------------------------------------------------------------------------------------------
   b) Hearing--------------------------------------------------------------------------------------------------------------
   c) Speech--------------------------------------------------------------------------------------------------------------
   d) Limbs----------------------------------------------------------------------------------------------------------------
   e) Vuneral l Diseases--------------------------------------------------------------------------------------------------
   f)Leprosy-------------------------------------------------------------------------------------------------------------
II. Neuroses-------------------------------------------------------------------------------------------------------------
III. Other serious disease---------------------------------------------------------------------------------------------

Date: ------------------------------------------------------------------ Signature: -----------------------------------------
Station: -------------------------------------------------------------- Designation: -------------------------------------

**Kiambatisho D**

## ORODHA YA VITABU VYA MASOMO


### a) VITABU VYA JIOGRAFIA:

1. Pritchard J.M. (1979), Africa a study Geography for Advanced students London Longman.
2. Msabila D. T (2003) Success in Geography climatology and Soil Science Dar es salaam – Afroplus Industries L.T.D.
3. Prichard J.M. (1990) Practical Geography for Africa, Longman.
4. Kamili, A Comprehensive Approach Practical Geography For Advanced Level, Dar es salaam, Afroplus Industries.
5. Kamili, Physical Geography for Africa, Dar es salaam Afroplus Industries.
6. Msabila D.T. Physical Geography, Dar es slaam Nyambari Nyangwine Publishers.
7. Msabila D.T. (2006) Human and economic Geography (Advanced level paper 2) Nyambali Nyangwine publishers

### b) GENERAL STUDIES: -

1. General studies Approach.
2. Richard, R.F. Mbalase. General Studies for Advanced Level Certificate;
3. Mgaywa, B.M. General Studies for Advanced level 3 rd Ed.
4. Joannes Bigirwa Mungu & Sospeter. M. Deogratias. Understanding Advanced Level general Studies; Advance Secondary SchoolEducation;

### c) VITABU VYA KEMIA

1. By S.chand,Conceptual Chemistry for class X Iand XII
2. By Tanzania Institute of Education, ADVANCED LEVEL INORGANIC CHEMISTRY part I and II.
3. Advanced chemistry review (2000-2012) 4.Ramsden, E.M (2000) A- level Chemistry, 4th Edition II.

### d) VITABU VYA BIOLOJIA

1. By Tayloratel (1999) Biological Science, third edition.Tong printing press Hongkong.
2. By Glenn and Tod,s (1999) Understanding Biology 4th Ed.Stanlye Thomes Ltd UK

### e) BASIC APPLIED MATHEMATICS.

1. Additional and Applied Mathematics by J. F.TALBERT
2. Basic applied mathematics (BAM) by Respicius Kiiza and Lugano Mwanginde
3. Basic applied mathematics review questions and solution